

MKATABA WA KUKODISHA SHAMBA

MKATABA huu umefanyika leo tarehe 21 Mwezi Novemba, Mwaka 2025.

Kati ya

MANASI KWIZERA MAJANJA wa S.L.P 472 Kahama, Mwenye Simu Na. 0759-301140 kwa upande mmoja (ambaye katika mkataba huu ataitwa "**MMILIKI**") neno ambalo litajumuisha yeye binafsi, warithi wake na wote watakaodai haki Kutokana na mkataba huu kwa upande mmoja.

Na

HAFEEZALI HYDERALI GANGJI wa Kahama, Mwenye Simu Na. 0754-279627 (ambaye katika mkataba huu ataitwa "**MKODISHWAJI**".) neno ambalo litajumuisha yeye binafsi, warithi wake na wote watakaodai haki Kutokana na mkataba huu kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mmiliki ni mmiliki halali wa Shamba lenye Ukubwa wa Ekari Kumi na Nne lililopo Kitongoji Mwabasabi, Kijiji cha Nyaligongo, Kata ya Mwakitolyo, katika Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Mkoa wa Shinyanga

NA KWA KUWA Mkodishwaji amemwendea Mmiliki kwa nia ya kutaka Kukodi Shamba hilo, kwa malipo ya kodi iliyokubaliwa katika mkataba huu na kwa mujibu wa masharti mengineyo yaliyoafikiwa kwenye mkataba huu;

NA KWA KUWA Mmiliki amekubali kumkodisha Mkodishwaji shamba hilo

HIVYO BASI, MKATABA huu unashuhudia na kuthibitisha kama ifuatavyo:

1. KWAMBA Mmiliki amemkodisha Mkodishwaji Shamba lililopo katika eneo lililotajwa hapo juu, kwa kodi ya Kiasi cha Shilingi Milioni Ishirini tu (Shs. 20,000,000/=) kwa Mwaka, ambayo inaanza leo tarehe 21/11/2025 mpaka tarehe 20/12/2026. Na Mmiliki kwa kusaini mkataba huu anakiri kupokea kodi ya Mwaka Mzima yaani Miezi Kumi na Mbili (12), ambayo ni sawa na Shilingi Milioni Ishirini tu (Shs. 20,000,000/=).
2. KWAMBA Mkodishwaji anaanza kukodi shamba hilo kuanzia leo tarehe 21 Mwezi Novemba Mwaka 2025 hadi tarehe 20 Mwezi Disemba Mwaka 2026, ambapo mkataba huu utakoma. Hata hivyo pande zote zinaweza kuingia mkataba mpya endapo itaonekana kuna umuhimu na uhiyari wa kufanya hivyo.
3. KWAMBA, kwa kuwa Mkodishwaji ametimiza masharti yote ya ulipaji kodi, Mmiliki anamkodisha Mkodishwaji shamba hilo bila kumuingilia katika kipindi chote cha upangaji huo.
4. KWAMBA Mkodishwaji anatakiwa atumie Shamba hilo kwa matumizi halali tu na si vinginevyo na yote haya yanafanyika pasipo kufanya shughuli nyingine yoyote batili katika Shamba hilo, na akifanya hivyo itakuwa ni kinyume cha sheria na taratibu za nchi.



5. KWAMBA Mkodishwaji haruhisiwi kukodisha shamba hilo alilokodishwa kwa mtu mwingine yeyote bila ya idhini kutoka kwa Mmiliki, na ikiwa Mkodishwaji atashindwa kuendelea na Mkataba basi Mkodishwaji atakabidhi shamba hilo kwa Mmiliki, lakini hawezi kurudishiwa sehemu ya kodi itakayokuwa imebaki.
6. KWAMBA Mpangaji na Mpangishaji wanaweza kusitisha mkataba huu kwa kutoa taarifa ya maandishi ya Mwezi mmoja.
7. KWAMBA kwa madhumuni ya mkataba huu, maneno "Mmiliki" na "Mkodishwaji" yatahusu familia, jamaa na wategemezi au warithi wa kila mmoja wao.

KWA USHUHUDA na UTHIBITISHO, mkataba huu umewekwa saini na Mmiliki na Mkodishwaji mbele ya shahidi kama inavyooneshwa hapa chini:

IMESAINIWA na Mmiliki ambaye ni
MANASI KWIZERA MAJANJA
 leo Tarehe 21 Mwezi Novemba, 2025



MMILIKI



Na kushuhudiwa na Shahidi, ambaye ni;

Jina: - GEORGE JOSEPH MAGUNANA
 Saini:

MBELE YANGU:
JINA: AUDAX HENRY RWECHUNGURA
SAINI
SIFA: WAKILI
ANUANI: S.L.P 472
TAREHE 21 NOVEMBA, 2025



IMESAINIWA na Mpangaji ambaye ni
HAFEEZALI HYDERALI GANGJI
 leo Tarehe 21 Mwezi Novemba, 2025



MKODISHWAJI

Na kushuhudiwa na Shahidi, ambaye ni;

Jina: -
 Saini:

MBELE YANGU:
JINA: AUDAX HENRY RWECHUNGURA
SAINI
SIFA: WAKILI
ANUANI: S.L.P 472
TAREHE 21 NOVEMBA, 2025

